JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU

# SERA BUNGE NA URATIBU

JARIDA LA MTANDAONI TOLEO LA TANO
May 2024



Mkutano wa kujadili hali na athari za mvua za el nino katika ukanda wa SADC.

KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 BARABARA YA POSTA 40412 DODOMA TANZANIA.

www.pmo.go.tz

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu Mhe. Jenista Mhagama ameshiriki katika Mkutano wa kujadili hali na athari za mvua za El Nino katika Ukanda wa SADC.

Mkutano huo ulifanyika kwa njia ya Mtandao (Zoom meeting) Jijini Dodoma ukihusisha Wizara za Kisekta zinazohusika na Masuala ya Kilimo, Maji, Nishati na Uratibu wa udhibiti wa Maafa ni maandalizi ya Mkutano wa dharura wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) Kuhusu Hali ya Mvua za El nino utakaofanyika kwa njia ya Mtandao Mei 20, 2024.



## Mradi wa kuendeleza lishe na ufugaji endelevu wa viumbe maji kwa wakulima wadogo yazinduliwa Mpitimbi



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya (Sera, Bunge na Uratibu), Mhe Jenista Mhagama amezindua Mradi wa kuendeleza lishe na ufugaji endelevu wa viumbe maji kwa wakulima wadogo (ARNSA) katika kijiji cha Mpitimbi

Mradi huo wa kuendeleza lishe na ufugaji endelevu wa viumbe maji kwa wakulima wadogo (ARNSA) unaoenda kutekelezwa katika Wilaya nne za Mikoa ya Ruvuma na Lindi na kulenga katika kunufaisha kaya elfu Moja (1000) katika Wilaya za Songea vijijini, Mbinga Mkoani Ruvuma, Ruhangwa na Mtama Mkoani Lindi,

ambapo pamoja na mambo mengine Familia na jamii hizo zinaenda kuinua hali ya maisha kwa kuongeza kipato na kuimalisha Lishe.

Akiongea katika uzinduzi wa mradi huo,Waziri Mhagama alisema Mpitimbi imebahatika kuanza na mradi huu, na kwakuwa Mkoa wa Ruvuma unaongoza kwa uzalishaji wa mazao ya chakula lakini, una changamoto ya udumavu,"Na ndiyo maana Serikali imeleta mradi huu ambao utatumia takribani zaidi ya shilingi Bilioni tatu nukta moja, katika maeneo tuliyojipangia, ambao ni sehemu ndogo tuu ya Programu kubwa ya kuendeleza sekta ya Kilimo na Uvuvi, Tumebahatika kuanza na mradi huu unaofadhiliwa na ubalozi wa Norway Nchini hivyo ni wakati mzuri wa Wilaya zitakazonufaika kuweza kujikimu kimapato na kiafya." Alisema.

Aliendelea kusema kuwa, kwa kuwa hali ya udumavu inaleta changamoto ya afya ya akili ni fursa sasa kwa wananchi wa mkoa wa Ruvuma kuendelea kuboresha afya, kupitia lishe ya viumbe maji na hasa Samaki.

Waziri Mhagama aliushukuru ubalozi wa Norway kupitia shirika lake la NORAD kuleta mradi huo mkoani Ruvuma, "Leo Tunazindua Shamba Darasa Ambalo linaenda kuchagiza maendeleo ya tabianzuri ya biashara na matumizi ya lishebora kupitia samaki wanaofugwa kwenye mabwawa, na miradi itakayofanywa kwenye baadhi ya halmashauri za Mkoa wa Ruvuma." Alisisitiza.

Alibainisha kuwa, Kupitia bwawa kubwa la Asili lililopo Mpitimbi ni wakati sahihi sasa wa kuimarishwa kwa bwawa hilo na kuanza kwa ufugaji mkubwa wa Samaki "Tunatamani kuona kuwa Bwawa hilo lenye ukubwa wa hekari 17.4 linaendelezwa na kuwa shamba Darasa." Alisema



## Kampuni ya Sanku, yapongezwa kwa kujikita katika urutubishaji wa vyakula nchini

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Bunge na Uratibu) Mhe. Jenista Mhagama amesema mahitaji ya virutubishi vya chakula ni ajenda kubwa ambayo itachochea katika kuongeza ajira kwa wakulima wetu na kuwa na uhakika na virutubishi tunavyovitumia hapa nchini.

Waziri amesema hayo alipotembelea na kukagua kiwanda cha Sanku kilichopo Mwenge Jijini Dar es salaam na kujionea maendeleo ya kiwanda hicho cha uchanganyaji wa virutubishi kwenye unga wa mahindi na ngano kwa bei nafuu.

Naomba muendeele kufanya ufutailiaji wa karibu katika kutoa elimu ili kuondoa matatizo mengine ya udumavu, utapiamlo na shida ya kupungukiwa vitamini A kwa wakinamama wajawazito.

"Hii kazi ni kazi yenye manufaa makubwa na itaweza kutusaidia sana kama nchi tuweze kusonga mbele na kusaidia kuitangaza nchi kwa kuwa na kiwanda kikubwa cha kuchanganya virutubishi," alisema Waziri Mhagama

Kwa upande wake Meneja Muandamizi wa Sanku Bw. Gwao Omari Gwao amesema kampuni yao inasaidia wafanyabishara wadogo na wakati kufanya urutubishaji ambazo zimefunguliwa katika Mikoa 26 Tanzania Bara na katika Halmashauri 142 Tanzania Bara.



.



## Ujenzi wa mji wa serikali Mtumba waridhisha

Serikali imesema hadi sasa watumishi wa umma 25,039 wamehamia Makao Makuu ya Nchi Jijini Dodoma pamoja na Taasisi 65 ambapo inaendelea na mpango kazi wa ujenzi wa Awamu ya Pili wa majengo ya Ofisi za Wizara na Taasisi unaotarajiwa kukamilika mwaka 2025.

Hayo yalisemwa Bungeni Jijini Dodoma na Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu, Mhe. Ummy Nderiananga wakati akijibu swali la msingi la Mbunge wa Bahi Mhe. Keneth Nollo aliyehoji ni lini mpango wa kuhamia Dodoma utakamilika na ni taasisi ngapi zimeshahamia mpaka sasa.

Mhe. Nderiananga alieleza kwamba Mpango wa kuhamisha Makao Makuu ya Serikali kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma ulianza rasmi mwaka 2016.

"Hadi sasa, jumla ya watumishi 25,039 kutoka Serikali kuu, Bunge, Mahakama, Vyombo vya Ulinzi na Usalama, pamoja na Taasisi 65 wameshahamia na wanaendelea kutekeleza majukumu yao wakiwa Dodoma. Pia Serikali inatarajia kukamilisha mpango wake wa kuhamia Dodoma kwa kuzingatia Mpango kazi Maalum wa ujenzi wa Awamu ya Pili ya ujenzi wa ofisi hizo,"Alisema Mhe. Nderiananga.



Kuhusu ujenzi wa nyumba za watumishi alibainisha kuwa Serikali ilianza ujenzi wa makazi rasmi ya viongozi kuanzia mwaka 2021/2022 kupitia Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ambapo nyumba 20 zilijengwa wakati hadi kufikia Mwezi Septemba mwaka 2023 nyumba za watumishi 150 ikiwemo nyumba ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Kwa sasa tuko kwenye zoezi la kupanga eneo ambalo tumelitoa kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za viongozi wa Serikali na watumishi wa umma tutakuwa na Ekari 4654 kati ya Mji wa Serikali Mtumba na Ikulu,"Alieleza Mhe. Nderiananga.

Aidha, aliwahakikishia Watanzania kwamba Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan inaendelea na mpango wake wa kuendeleza Mji wa Serikali- Mtumba kama ilivyokusudiwa.

Dkt. Yonazi asisitiza kuwekwa anwani za makazi nyumba zinazojengwa Hanang'



Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia masuala ya Sera, Bunge na Uratibu Dkt. Jim Yonazi ametembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa nyumba 108 za waathirika wa maafa ya maporomoka ya mawe, tope na miti kutoka mlima Hanang' yaliyotea Wilayani Hanang' Mkoani Manyara mwishoni mwa mwaka Jana, 2023.

Dkt. Yonazi amefanya ziara hiyo mwishoni mwa wiki ambapo pamoja na mambo mengine amesisitiza uwekaji wa mifumo ya anwani za Makazi katika nyumba hizo zitakazoonesha namba za nyumba na vibao vyenye majina ya mitaa kurahisisha utambuzi wa makazi na wakazi husika ili kurahisisha ufikishaji wa huduma na bidhaa mahali stahiki na kuchagiza maendeleo kwa wananchi hao.

Dkt. Yonazi ametoa maagizo hayo ya kuweka anwani za makazi kwa kuzingatia umuhimu wake katika nyumba hizo zinazojengwa katika eneo la Gidagamowd lililopo katika Kitongoji cha Waret Wilayani Hanang mkoani humo.

Alisema kuwa Serikali imetenga eneo la ekari 100 ambapo jumla ya viwanja 269 vimepimwa ambapo kati ya hivyo, viwanja 226 ni makazi pekee, viwanja 26 ni makazi na biashara na viwanja 17 ni maeneo ya huduma za kijamii.

Aidha amewata wakandarasi kukamilika utekelezaji wa mradi husika kwa wakati na kuzingatia ubora unaotakiwa.

“Mradi ukamilike kwa wakati kama ilivyokubalika yaani ndani ya siku tisini na uendane na thamani ya fedha itakayotumika pamoja na hilo endeleeni kushirikiana na wenyeji wa eneo hili ili kuimarisha mahusiano na wazawa,” alisisitiza Dkt. Yonazi

Akizungumza kuhusu maendeleo ya mradi huo Kaimu Operesheni Kamanda Luteni Kanali Ashraf Hassan ameahidi kuhakikisha kuwa maelekezo yaliyotolewa na Dkt. Yonazi yanafuatwa ili ujenzi ukamilike kwa wakati.

Luteni Kanali Ashraf amemueleza Katibu Mkuu kuwa ujenzi huo wa nyumba 73 umefikia asilimia 40, na unajengwa kwa kuzingatia vigezo vya ubora uliokusudiwa na Serikali.

"Tumefurahi kutembelewa na Katibu Mkuu Dkt. Yonazi ambaye ameeleza kuridhishwa na maendeleo ya mradi, na sisi tunamuahidi kuwa ujenzi huu utakamilika kwa wakati lakini pia kwa kuzingatia viwango vya ubora vilivyoelekezwa" amesema Luteni Kanali Ashraf

"Tumefurahi kutembelewa na Katibu Mkuu Dkt. Yonazi ambaye ameeleza kuridhishwa na maendeleo ya mradi, na sisi tunamuahidi kuwa ujenzi huu utakamilika kwa wakati lakini pia kwa kuzingatia viwango vya ubora vilivyoelekezwa" amesema Luteni Kanali Ashraf



Wadau waombwa kushirikiana na serikali kukabiliana na utapiamlo

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, (Sera, Bunge na Uratibu) Dkt. Jim Yonazi ametoa rai kwa wadau wa sekta binafsi kushirikiana serikali katika kukabiliana na swala la utapiamlo nchini.

Ametoa kauli hiyo Jijini Dar e Salaam wakati kikao kilichohusisha wadau wa sekta binafsi katika kujadili maandalizi ya Mkutano wa 10 wa lishe unaotarajiwa kufanyika Jijini Mwanza Mwezi Septemba.

Ametoa kauli hiyo Jijini Dar e Salaam wakati kikao kilichohusisha wadau wa sekta binafsi katika kujadili maandalizi ya Mkutano wa 10 wa lishe unaotarajiwa kufanyika Jijini Mwanza Mwezi Septemba.

"Lazima tuunganishe nguvu tukabiliane na changamoto ya udumavu katika Jamii yetu ili kampuni zetu za ndani ziweze kuendelea katika ushindani na kampuni za nje," alihimiza

Aidha sekta binafsi imepata nafasi ya kutambulika na kushikana mkono na

Kwa upanda wake Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania Dkt. Germana Leyna amesema sekta binafsi wanayo nafasi ya kuhamasisha walaji katika kujenga hamasa ya kuleta mabadiliko chanya katika lishe kulingana na bidhaa zinazozalishwa.

"Tatizo la utapiamlo lisipopatiwa ufumbuzi, linaweza likapunguza nguvu ya ununuaji (Purchasing Power) hata kama bidhaa zitakuwa bora na muhimu,"

Alibainisha.

Naye Bw. Ally Sechonge kutoka kampuni ya Tanga Freshi amesema kwa mujibu wa takwimu za Bodi ya maziwa ni 4% ya Maziwa yanayotoka kwa Ng'ombe ndio yanayosindikwa na 96% yananywewa bila kusindika.

"Tatizo kubwa ni kwamba walaji wanakuwa na maamuzi jinsi gani watatumia fedha yao, bila kuzingatia swala la utaratibu mzuri wa kula," alisema.

Naye Bw. Iddi Mvungi kutoka kutoka kampuni ya Bakhresa ameishukuru serikali kwa kujumuisha sekta binafsi katika mapambano dhidi ya utapiamlo.

Sisi tunaendelea kuihakikisha serikali kwamba tutakuwa pamoja na Serikali na kwa kuhakikisha maelekezo yote yanayoelekweza, tunayazingatia katika uzalishaji wa bidhaa.



Jarida la Mtandao limeandaliwa na kutolewa na kitengo cha Mawasiliano Serikalini Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera Bunge na Uratibu.



KATIBU MKUU
OFISI YA WAZIRI MKUU
2 MTAA WA RELINI , S.L.P 980
40480 DODOMA
Baruapepe, ps@pmo.go.tz, simu, +255262322480
Fax;255262324534, Tovouti;www.pmo.go.tz